المجلس الأعلى للشئون الإسلامية بتنزانيا
BARAZA KUU LA WAISLAM TANZANIA ( BAKWATA )
THE NATIONAL MUSLIM COUNCIL OF TANZANIA
**P.O.BOX 21422 PHONE: 0717082543/0717011207, DAR ES SALAAM**

**FOMU Na. 2**

**FOMU YA MAOMBI YA KUKODISHA ENEO LA BIASHARA/OFISI KATIKA JENGO LA KITEGA UCHUMI LA BAKWATA COMMERCIAL COMPLEX BUKOBA MANISPAA**




Ofisi ya Katibu Mkuu wa Baraza Kuu la Waislam Tanzania **(BAKWATA)**, wa **S.L.P. 21422, Simu; 0754 453 200/ 0717 082 543/ 0629 310 310/ 0713 350 310 Dar es salaam**. Anawatangazia na kuwakaribisha wadau na wafanyabiashara wote waliochukua fomu za awali kwa nia ya kuomba maeneo au nafasi za kufanya biashara katika jengo letu la **BAKWATA COMERCIAL COMPLEX BUKOBA MANISPAA**, wafike katika ofisi za Bakwata Wilaya Bukoba Manispaa kwa ajili ya kupatiwa fomu namba mbili **(No.2)** yenye maelekezo maalum kwa wateja wetu wote.

Kwa waombaji walio karibu na eneo la Mradi wafike moja kwa moja katika Ofisi za **BAKWATA** Wilaya Bukoba Manispaa au wawasiliane na Katibu Bakwata Wilaya kupitia simu Na. **0756074626** kwa ajili ya kupatiwa fomu husika, na wateja wengine watapatiwa fomu kupitia mtandaoni na Kundi la ujenzi na la wateja.

Mwombaji atatakiwa kuyasoma na kuyaelewa vema maelekezo yaliyomo kwenye fomu ili ajiridhishe kuwa anakidhi vigezo vilivyowekwa na baada ya hapo atalazimika kulipia ada ya maombi ya kiasi cha shilingi Hamsini elf tu (50,000) au kiasi cha shilingi laki moja tu (100,000) kwa wafanya biashara wakubwa **(wateja wakubwa ni wale wanaoomba zaidi ya mita za mraba 51 Sqmt)**, kiasi ambacho hakitarejeshwa ili fomu yake iweze kujadiliwa, kinyume chake ni kwamba fomu ambayo haitalipiwa moja kwa moja haitaingizwa kwenye kinyang'anyiro cha kujadiliwa.

Kwa mujibu wa mwongozo na maelekezo ya fomu hii, mwombaji anatakiwa kuambatanisha vielelezo vyote vinavyotakiwa kwa ajili ya uhakiki wa biashara yake anayokusudia kufanya katika eneo analoomba.

Maeneo tuliyonayo ni ya ukubwa tofauti kuanzia mita za mraba **25, 50, 100, 200, 300, 400** na zaidi kulingana na mahitaji ya mteja. Baadhi ya maeneo yaliyotengwa ni kwa ajili ya biashara kama vile **Maduka makubwa ya jumla, Maduka ya kati, Maduka madogo, Mgawaha, ATMS, Shule, Poly clinic na Kumbi za Mikutano N.K**

2. Ukubwa wa eneo unaloomba kwa mahitaji ya matumizi ya bishara yako kwa kipimo cha mita za Mraba **(Sqmt)**: sqmt
Kwakuwa kila mteja atasajiliwa na kupewa eneo lake kwa biashara moja tu, na kwakuwa mteja hataruhusiwa kuchanganya au kufanya biashara tofauti na biashara alioiombea eneo, basi mwombaji aeleze wazi aina ya biashara halisi anayotarajia kufanya katika eneo husika

4. Mteja atakaye pokelewa na kukubalika ni yule tu mwenye biashara zilizo sajiliwa na Serikali au mamlaka husika. Kwa msingi huo, mwombaji anahitajika kuambatanisha nyaraka za usajiliwa wa biashara zake **(Legal Trading documents)** Pamoja na vibali kutoka kwenye mamlaka husika, ikiwa biashara zake zitakuwa zinahusishwa na vibali husika.

**5. Baadhi ya nyaraka muhimu zinazotakiwa kuambatanishwa Pamoja na fomu hii, ni kama zifuatazo:-**

A) Kwa Makampuni ambatanisha (i) Cheti cha Usajili wa Kampuni **(Certificate of Incorporation)**, (ii) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN), na **(VAT)** kama Kampuni imejisajili na **(VAT)**, (iii) **Leseni hai ya Biashara**, (iv)Taarifa ya Benki ya **(Bank statement)** angalau ya miezi sita (6), (v) Takaso la kodi/**Tax Clearance Certificate**, (vi) Kadi ya utambulisho wa uraia **(NIDA)** kwa wakurugezi wa Kampuni.
B) Kwa waombaji wenye usajili wa jina la bishara **(SOLE PROPRIATOR)** wataambatanisha nakala za nyaraka kama hizo zilizotajwa kwenye kipengele **(A)** ikiwemo ziada ya cheti cha **(Extract from the Registrar)**
C) Kwa wafanya biashara binafsi (i) Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi **(TIN)**, na **(VAT)** kama umejisajili na VAT, (ii) Leseni hai ya Biashara, (iii)Taarifa ya Benki ya **(Bank statement)** angalau ya miezi sita (6), (iv) Takaso la kodi/Tax Clearance Certificate, (v) Kadi ya utambulisho wa uraia **(NIDA)** ya mwombaji.
Endapo muombaji atakidhi vigezo vya kupewa eneo mara moja atapewa taarifa ya wito kuja kuonyeshwa sehemu ya eneo lake atakalo fanyia biashara, kisha atalazimika kulipia mara moja malipo ya kodi ya mwaka mmoja ndani ya siku saba toka tarehe kuarifiwa na malipo yote ya ununuzi wa fomu yatalipwa kupitia **Banki ya CRDB** akaunti nambari **015C522704600 BAKWATA UJENZI ACCOUNT**.
Mwobaji wakati kurejesha fomu atawasilisha kwa Pamoja stakabadhi ya malipo ya malipo ya fomu kinyume cha hivyo fomu zake hazitapokelewa wala kujadiliwa.
Kwamba, baada ya kukamilisha malipo ya pango atapewa na kusaini mkataba wa pango lake, kisha atakabidhiwa eneo lake la pango na atapewa kipindi cha muda wa mwezi mmoja wa maandalizi **(Gres period)** kabla ya kuanza kukatwa au kuhesabiwa kodi yake na baada kipindi hicho cha mwezi mmoja kodi itaanza kuhesabiwa na kukatwa hata kama mteja atakuwa bado hajaanza kufanya biashara zake.